SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jarida la

# RELI NA MATUKIO

Toleo namba 30, Juni 2023

Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

# MABEHEWA SITA YA GHOROFA YA TRENI YA KISASA YAPOKELEWA



Na Mwandishi wetu.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Atupele Mwakibete apokea mabehewa sita (6) ya ghorofa yatakayotumika katika uendeshaji wa treni ya kisasa ya reli yenye kiwango cha kimataifa - SGR, kwenye hafla fupi iliyofanyika katika viwanja vya bandari jijini Dar es Salaam Juni 9, 2023.

Mabehewa yaliyopokelewa ni sita (6) kati ya mabehewa thelathini (30) ya abiria yaliyonunuliwa na kufanyiwa maboresho na Kampuni ya Lueckemeier Transport and Logistic ya Ujerumani.

Inaendelea Uk. 2

## SGR TANZANIA YAWA KIVUTIO KATIKA MAADHIMISHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA BARANI AFRIKA Uk. 3




Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora Mhe. Ridhiwani Kikwete akitoa maelezo kwa wadau wali otembelea banda la TRC katika maonesho ya wiki ya utumishi wa umma barani Afrika yaliyofanyika, Victoria Falls, nchini Zimbabwe, Juni 2023.

# MABEHEWA SITA YA GHOROFA YA TRENI YA KISASA YAPOKELEWA



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Atupele Mwakibete akikagua moja ya mabehewa sita ya ghorofa kwaajili ya SGR mara baada ya kupokea mabehewa hayo katika bandari ya Dar es Salaam, Juni 2023.

**Inatoka Uk. 01**

Mhe. Mwakibete amesema kuwa Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania ina matarajio makubwa ya kukamilisha ujenzi wa reli ya kisasa - SGR kwa haraka na ufanisi mkubwa ili kuweza kutoa huduma za usafiri wa reli kwa makusudio ya kukuza uchumi wa nchi na maendeleo ya jamii kwa ujumla .

"Serikali ya awamu ya sita ilishaanza mchakato wa ununuzi wa mabehewa ya abiria na mizigo tumeshapokea mabehewa mapya 14 kati ya 59 kutoka nchini Korea Kusini na leo tunapokea mabehewa sita ya ghorofa kwaajili ya kuanza majaribio katika kipande cha kwanza cha mradi wa SGR pindi kichwa kimoja cha treni kitapowasili mwezi Julai mwaka huu" alisema Mhe. Mwakibete.

Mkurugenzi Mkuu Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa amesema mabehewa sita ya ghorofa yaliyopokelewa manne ni ya daraja la pili yenye uwezo wa kubeba abiria mia ishirini na tatu (123) na mabehewa mawili ni ya daraja la tatu yenye uwezo wa kubeba abiria mia na arobaini (140).

"Behewa moja lina uwezo wa mabasi matatu na lina mwendokasi wa kilomita mia sitini (160) kwa saa, ndani ya mabehewa kuna kiyoyozi, Runinga na CCTV kwaajili ya usalama wa abiria na mizigo" alisisitiza Ndugu Kadogosa.

Naye Msemaji wa Serikali Ndugu Gerson Msigwa alisema mabehewa haya ya ghorofa ni ya historia kwa Tanzania, tangu nchi ipate uhuru ndiyo mara ya kwanza tunapokea mabehewa ya ghorofa.

"Hongera TRC Pamoja na maneno ya watu wachache mwenyenia ya kutuharibia lakini kazi inaendelea" alisema Ndugu Msigwa

Mhe. Edward Mpogolo Mkuu wa Wilaya ya Ilala alipotoa salamu za Mkoa wa Dar es Salaam kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam amesema Treni ya SGR itaanza safari zake Dar es Salaam jiji la biashara lenye wakaazi zaidi ya milioni tano itakuwa ni chachu ya kukuza uchumi.

"Sisi ni mashuhuda wa ujenzi wa reli ya viwango vya kimataifa inayojengwa na serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, pongezi kwa TRC kwa kazi nzuri, na Uongozi wa Mkoa utaendelea kutoa ushirikiano kwenye ujezi wa mradi wa SGR" alisema Mhe. Mpogolo.

Wizara ya ujenzi na uchukuzi kupitia Shirika la Reli Tanzania linaendelea kusimamaia ununuzi wa mabehewa ya abiria, vichwa vya treni, mabehewa ya mizigo 1430 na mitambo ya ukarabati wa njia ya reli ya SGR ili kuhakikisha inaboresha usafiri na usafirishaji wa mizigo kwa njia ya reli ya kisasa.

Mhe. Mwakibete amesisitiza nia ya Serikali ya awamu ya sita ni kuhakikisha inaunganisha Bahari na Maziwa yote hapa nchini kwa njia ya SGR.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Atupele Mwakibete akipata maelezo kutoka kwa Mhandisi Kelvin Kimario kuhusu mabehewa sita ya ghorofa kwaajili ya SGR yaliyowasili nchini Juni 2023.

# SGR TANZANIA YAWA KIVUTIO KATIKA MAADHIMISHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA BARANI AFRIKA



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti, Utumishi wa umma na Utawala bora Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete akifafanua jambo kuhusu Eneo huru la biashara katika bara la Afrika kuhitaji utawala wa umma barani Afrika, uwekazaji mpya katika kurahisisha ufanisi wa rasilimali watu kwa kutumia teknolojia mbalimbali za mifumo katika mkutano wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma Barani Afrika, Victoria Falls, Zimbabwe Juni 2023

**Na Mwandishi wetu TRC**

Mradi wa ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa(SGR), unaoendelea nchini Tanzania kuwa kivutio kwa Nchi mbalimbali barani Afrika zilizoshiriki katika maonesho ya maadhimisho ya wiki ya utumishi wa umma yaliyofanyika Victoria Falls, Zimbabwe kwa mara ya tisa tangu kuasisiwa. Maonesho yameanza tarehe 21 Juni hadi 23, 2023.

Shirika la Reli Tanzania (TRC) ni miongoni mwa taasisi za Serikali ziliyofanikisha ushiriki katika maonesho ya maadhimisho ya wiki ya utumishi wa umma barani Afrika. Maonesho hayo yamebeba dhima chini ya kaulimbiu kuu isemayo "Eneo Huru la Biashara katika Bara la Afrika litahitaji Utawala wa Umma wenye nia madhubuti ili kufanikiwa" (The African continental Free Trade Area Will Require a Fit for purpose African Public Administration to Succeed).

Tofauti na kauli mbiu kuu maadhimisho yameambata na na kauli mbiu ndogo ambazo ni Diplomasia iliyoimarika, kuoanisha mifumo ya sheria na ushirikiano wa kikanda , kuzuia uhalifu unaovuka mipaka kwa usimamizi mzuri wa uratibu na utekelezaji wa mamlaka ya eneo huru la biashara Afrika, Utawala wa umma uliostawi na kutengeneza mazingira wezeshi ya uwekezaji katika viwanda vya kuongeza thamani ili kuongeza faida za muundo wa eneo huru la biashara Afrika.

Kuanzisha teknolojia mpya na muhimu katika usimamizi, ufundi, ujuzi wa kijasiliamali ili kuhakikisha matumizi mazuri ya rasilimaliwatu, fedha na nguvu kazi kupata matokeo chanya ya biashara za kuvuka mipaka. Hizi zote ni miongoni mwa mada zilizojadiliwa katika mkutano wa maadhimisho ya wiki ya utumishi wa umma barani Afrika,Victoria Falls, Zimbabwe.

Kutokana na teknolojia mpya ya uwekezaji inayoendelea Nchini Tanzania katika kuimarisha sekta ya miundombinu ya reli kwa ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa ( SGR) imekua kivutio kwa washiriki wa maonesho ya maadhimisho kwa kuwa uwekazaji huu utaleta matokeo chanya katika biashara za kuvuka mipaka kwa nchi mbalimbali za Afrika.

Kupitia sera ya taifa na mkakati wa nchi kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 ni Dhahiri kwa taifa kuwa na miundombinu imara na yenye ufanisi kwa kutumia teknolojia mpya ya SGR itachochea utoaji wa huduma bora ya usafirishaji kwa haraka na kwa bei nafuu.

Inaendelea Uk. 04

# SGR TANZANIA YAWA KIVUTIO KATIKA MAADHIMISHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA BARANI AFRIKA



Naibu Waziri wa Nchi,Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa umma na Utawala bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (wa pili kulia) na watumishi wa TRC wakifurahi baada ya kupokea zawadi ya mshindi wa pili katika maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma Afrika, Victoria Falls, Zimbabwe Juni 2023.

Inatoka Uk. 03

Ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa (SGR) ni nguzo kubwa katika kuchochea na kupunguza gharama na muda wa safari kwa abiria na mizigo. Mataifa yenye nguvu duniani yamejengwa nakujikita katika kuwa na miundombinu imara kwenye utoaji wa huduma za usafiri kwa haraka kutoka mji mmoja hadi mwingine.

Tanzania ni kati ya nchi chache ambazo ni mlango wa nchi zingine katika kupitisha bidhaa kwenda na kutoka, hii ni fursa kubwa kwa taifa kuwekeza kwenye miundombinu imara ya usafirishaji kwa wakati, salama na kwa bei nafuu na dhima hii imekua kivutio zaidi kwa maonesho yaliyofanyika Victoria Falls, nchini Zimbabwe.

Usafiri wa reli hupunguza gharama ya bidhaa kwa asilimia kati ya 30% hadi 40% na huchochea kwa kiasi kikubwa uchumi, kuwekeza katika ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa Tanzania pia kunakwenda kuleta maendeleo ya watu na jamii kwa ujumla.

Awamu ya kwanza ya Ujenzi wa SGR ni Dar es Salaam – Mwanza na itaunganisha mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma (makao makuu), Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza na Nchi za maziwa makuu Kama Uganda, Rwanda, Congo na Burundi. Biashara za kuvuka mipaka kwa nchi mbalimbali imekua dhima kuu katika majadiliano kipindi cha mkutano wa maadhimisho ya wiki ya utumishi barani Afrika.

Awamu ya pili ya ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa (SGR) unaendelea Tabora – Kigoma, na baadaye Kaliua – Mpanda – Karema pamoja na nchi za Congo, Burundi na Rwanda. Kupitia maendeleo ya ujenzi wa reli ya kisasa nchini Tanzania imekua kivutio katika maonesho ya wiki ya utumishi wa umma nchini Zimbabwe.

Mwakilishi Mkuu katika maadhimisho ya wiki ya Utumishi wa umma barani Afrika kutoka Tanzania Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ua Utumishi wa Umma na utawala bora Ridhiwani Kikwete, alipata fursa ya kuchangia katika kikao cha maadhimisho ya wiki ya Utumishi wa Umma barani Afrika kuhusu maendeleo ya biashara huru kwa nchi za Afrika pia alielezea uboreshaji wa miundombinu ikiwemo reli na barabara kuhakikisha utumishi wa umma unakuwa na tija ili kutimiza malengo ya bara la Afrika.

Naibu Waziri aliongeza kuwa miundombinu mbalimbali imeweza kufanyiwa kazi nchini Tanzania kwa kuanza na ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa (SGR) katika kuwezesha mawasiliano kati ya nchi za maziwa makuu. SGR itapokamilika itawezesha nchi kama Uganda, Rwanda, Congo na Burundi kufikiwa kirahisi na kupunguza muda na gharama za usafirishaji mizigo, pia nchi jirani zitaendelea kujifunza teknolojia mpya ya ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa nchini Tanzania kwakuwa viongozi wa nchi mbalimbali za Afrika kama Uganda, Zambia na Kongo tayari wameshakuja kujifunza na kushuhudia uwekezaji wa SGR nchini.

Tanzania iko katika mchakato wa kujenga chuo kitachotoa Elimu ya teknolojia hii mpya ya reli ya SGR ili kuendeleza rasilimali watu ambao watakua na uwezo wa kujenga, kuendesha na kukarabati endapo kutakua na changamoto. Naibu Waziri alisisitiza kuendelea kuimarisha Diplomasia ya uchumi kwa nchi za Afrika, Umoja na ushirikiano.

Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma Barani Afrika yalifikia kilele Juni 23, 2023. Ushiriki wa Tanzania katika maadhimisho ya wiki ya utumishi wa umma barani Afrika unasaidia kujipambanua kidiplomasia katika Utawala Bora na utekelezaji wa maadhimio yatakayokubaliwa utaisaidia Tanzania kuchangia ufikiwaji wa maono ya kuwa na Eneo Huru la Biashara Barani Afrika.

# YALIYOJIRI KATIKA MAONESHO YA WIKI YA UTUMISHI AFRIKA, VICTORIA FALLS ZIMBABWE



Naibu Waziri wa Nchi,Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa umma na Utawala bora Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete akiwa katika picha na watumishi wa taasisi mbambali kutoka Tanzania zilizoshiriki maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma Barani Afrika, Victoria Falls, Zimbabwe hivi karibuni Juni 2023.



Naibu Waziri wa Nchi,Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa umma na Utawala bora Mhe. Ridhiwani Jakaya Mrisho Kikwete akipata maelezo kutoka kwa Bwana Oclay Frank kuhusu uwekazaji wa Teknolojia mpya katika kurahisisha ufanisi wa rasilimali watu kwa kutumia teknolojia mbalimbali katika Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma Barani Afrika, Victoria Falls, Zimbabwe Juni 2023.




Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa umma na Utawala bora Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete akipata maelezo kutoka kwa Mhandisi Adam Kimbewele (kulia) kuhusu Teknolojia mpya ya ujenzi wa SGR katika Banda la TRC wakati wa maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma Barani Afrika, Victoria Falls, Zimbabwe Juni 2023.




Picha ya pamoja Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa umma na Utawala bora Mhe. Richiwani Jakaya Kikwete (aliyeketi wa tatu kulia) pamoja na viongozi wengine mbalimbali kutoka nchi za bara la Afrika walioshiriki katika maadhimisho ya wiki ya utumishi wa umma barani Afrika yaliyofanyika, Victoria Falls, Zimbabwe. Juni 2023



Mabehewa Sita (6) ya Ghorofa kwaajili ya reli yenye kiwango cha kimataifa - SGR yaliyowasili Bandari ya Dar es Salaam kutoka nchini Ujerumani Juni 6, 2023



Mafundi wakiendelea na uzalishaji wa mataruma yanayotumika katika ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa - SGR kipande cha tano Mwanza - Isaka katika kambi ya Seke mkoani Shinyanga, Juni 2023.



Kazi ya kujaza udongo katika tuta ikiendelea wakati wa usiku katika kipande cha tano cha mradi wa ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa - SGR Mwanza - Isaka, Juni 2023.



Kazi ya kuweka mataruma ikiendelea katika kipande cha tano cha mradi wa ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa - SGR Mwanza - Isaka, Juni 2023.



Wataalamu wakipima upana wa shimo kwaajili ya ujenzi wa msingi wa nguzo ya umeme katika tuta la reli yenye kiwango cha kimataifa - SGR akipande cha tano Mwanza - Isaka, Juni 2023.

# BODI PPRA YARIDHISHWA NA VIWANGO VYA MRADI WA SGR



Meneja msaidizi mradi wa SGR Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi David Mausa (kushoto) akiwaeleza wajumbe wa bodi ya wakurugenzi PPRA kuhusu chumba cha kuongozea treni za kisasa walipotembelea mradi katika jengo la stesheni jijini Dar es Salam, Juni 2023.



Kaimu Mkurugenzi wa Ishara, Mawasiliano na Umeme Mhandisi Mateshi Titto (wa tatu kushoto) akitoa maelezo ya mradi wa SGR morogoro - Makutupora kwa bodi ya wakurugenzi kutoka PPRA walipotembelea jengo la stesheni ya SGR jijini Dodoma, Juni 2023.

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania limepokea ugeni wa bodi ya wakurugenzi kutoka Mamlaka ya Udhibiti Ununuzi wa Umma - PPRA ambapo wamefanya ziara ya siku mbili kutembelea ujenzi wa mradi wa reli ya kisasa - SGR kutoka Dar es Salama hadi Dodoma hivi karibuni Juni, 2023.

Bodi ya wakurugenzi kutoka PPRA imetembelea mradi wa SGR kwa lengo la kukagua na kujiridhisha juu ya thamani ya fedha iliyotumika kukidhi viwango vinavyotakiwa katika kujenga mradi huo mkubwa wa kimkakati.

Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi kutoka PPRA Dkt. Leonada Mwagike ameeleza kuwa ujenzi wa mradi wa SGR umekidhi viwango na ubora utakaowezesha usafirishaji wa abiria na mizigo kwa muda mfupi na treni kufika sehemu kwa wakati.

"Tumeona ubora wa ujenzi uliowekezwa katika mradi huu na nimefurahishwa kwakuwa watanzania wengi wana ujuzi wa kuusimamia mradi huu mkubwa" alisema Dkt. Mwagike.

Naye Mtendaji Mkuu kutoka PPRA Bw. Eliakim Maswi alisema kuwa fedha za umma zinatakiwa zitumike kulingana na maelekezo na Sheria iliyopo hivyo maendeleo ya mradi huo unaenda sambamba na thamani ya fedha iliyowekwa na Serikali.

"PPRA jukumu lake ni kukagua na kuona matumizi yaliyotumika yanalingana na thamani ya fedha iliyowekwa, vitu vilivyofanywa katika mradi huu ni vikubwa sana" alisema Bw. Maswi.

Mkurugenzi Mkuu kutoka TRC Ndugu Masanja Kadogosa ametoa shukurani kwa bodi ya wakurugenzi kutoka PPRA kwa kutembelea mradi wa SGR na kuona maendeleo ya mradi pamoja na kujiridhisha katika maeneo mbalimbali.

"Inatoa picha nzuri kwa kile walichokiona kwenye makaratasi na kuhakiki ujenzi uliofanyika hivi sasa. PPRA kwetu ina umuhimu sana kwa maana ya manunuzi tunafuata Sheria za PPRA" alisema Ndugu Kadogosa.

Naye Mjumbe wa bodi ya wakurugenzi kutoka PPRA mhandisi Sylvester Mayunga alisema kuwa reli ya kisasa imejengwa kwa viwango na ubora mkubwa kwa kujenga njia iliyonyooka na kudhibiti sehemu korofi zenye maji kwa kupitisha reli kwenye mahandaki.

"Usimamizi umekuwa mzuri na tumeona vitu vingi vipo imara kuanzia mataruma, kuweka vitu vya kudhibiti wizi na hujuma kwenye njia ya reli " alisema Mhandisi Mayunga.

Mradi wa SGR kipande cha kwanza kutoka Dar es Salaam - Morogoro kimefikia 98.26% na kipande cha pili kutoka Morogoro - Makutupora 94.19%.

# KASI YA UJENZI SGR YAENDA SAMBAMBA NA UTWAAJI ARDHI



Na Mwandishi wetu

Shirika la Reli Tanzania – TRC linaendelea na shughuli za ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa – SGR awamu ya kwanza na ya pili sambamba na utwaaji ardhi katika maeneo mbalimbali nchini ili kupisha mradi ikiwemo mkoani Singida na Tabora, Juni 2023.

Lengo la utwaaji ardhi ni kukabidhi maeneo kwa mkandarasi wa mradi wa SGR kipande cha tatu Makutupora – Tabora ili aweze kuendelea na ujenzi wa mradi na kukamilisha kwa muda uliopangwa. Zoezi linaendelea mkoani Singida na Tabora ambapo zaidi ya wananchi 200 waliotwaliwa maeneo yao na baadaye kufanyiwa uthamini wanalipwa fidia ili kupisha mradi.

Maeneo ambayo wananchi wamelipwa fidia katika wilaya za Tabora, Uyui, Sikonge, Manyoni na Itigi ni pamoja na Makutupora, Saranda, mabondeni, Tambuka Reli, Kipondola, Aghondi, Kitopeni, Kazikazi, Tura, Karangasi, Nyahua, Kamama, Igalula, Itulu, Milembela na Chang'ombe.

Maeneo yaliyotwaliwa ni kwaajili ya kuchimba kifusi, kutupa kifusi na maeneo ya kuzalisha kokoto. Wananchi waliotwaliwa maeneo wamelishukuru Shirika kwa kuharakisha kulipa stahiki zao na wameonesha imani kubwa kwa Serikali kuwa miradi ya kimkakati inakwenda kuleta maendeleo hivyo wananchi wanapaswa kuendelea kutoa ushirikiano.

"Shirika la Reli kupitia mradi wa SGR wameweza kutwaa sehemu ya eneo langu kwaajili ya kuchimba kifusi lakini nachopenda kushukuru ni kwamba wamejitahidi kufanya kila liwezekanalo kulipa fidia. Kwahiyo leo nashukuru wamenipa hundi yangu, naomba wananchi wote kwa maeneo haya ambayo yanatwaliwa watoe ushirikiano mradi uweze kupita na maendeleo yapatikane" alisema bwana Anselim Tendwa. Mkazi wa Itulu, Tabora.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyahua Bwana Abdallah Katoto amesema kuwa "Serikali inajitahidi kuboresha maisha ya wananchi wake, nashukuru leo imekuja kulipa fidia ili kupisha mradi huu wenye manufaa, hapa (Nyahua) kutakuwa na Stesheni ni suala ambalo wananchi wa wilaya ya Sikonge walikuwa wanalitaka, hivyo wanaishukuru Serikali kwasababu Stesheni hii itaunganisha Sikonge na mikoa ya jirani ikiwemo Mbeya na Katavi".

Zoezi la ulipaji fidia ni endelevu katika maeneo ambayo mradi wa SGR umepita, linafanyika kwa kufuata taratibu na Sheria ikiwemo Sheria ya Uthamini na Sheria ya Fidia ambapo viongozi wa maeneo husika na wananchi wanahusishwa kuanzia mchakato wa kutambua maeneo, uthamini, utoaji taarifa hadi utoaji fidia.

## MCHAKATO WA UNUNUZI WA MABEHEWA YA SGR NA MATUMAINI YA KUANZA UENDESHAJI SGR

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania limepewa dhamana ya kusimamia na kuendeleza sekta ya usafiri wa reli nchini. TRC inaendelea kusimamia vyema ujenzi wa reli ya kimkakati ya kimataifa ya SGR, kwa awamu ya kwanza yenye vipande vitano (5) na ujenzi unaendelea katika hatua mbalimbali.

Kipande cha kwanza cha kutoka Dar Es Salaam – Morogoro ujenzi umefika asilimia 98, kipande cha pili Morogoro - Makutupora ujenzi umefika asilimia 94, kipande cha tatu Makutupora - Tabora ujenzi umefika asilimia 7, kipande cha nneTabora - Isaka ujenzi umefika asilimia 3 na kipande cha mwisho Mwanza – Isaka ujenzi umefika asilimia 33.

Serikali ya Tanzania imeshasaini mkataba wa ujenzi wa SGR (Standard Gauge) kipande cha sita kutoka Tabora hadi Kigoma, tarehe 20.12.2022 yenye urefu wa kilomita 506 , njia kuu ni kilomita 411, mapishano ni kilomita 95. Reli ya kisasa imekusudiwa kupunguza msongamano wa malori barabarani ili kukuza uchumi wa nchi kupitia usafirishaji wa haraka na nafuu wa mizigo.

Katika hatua zote za ujenzi na matayarisho ya kuanza kwa shughuli za majaribio na uendeshaji wa SGR. Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania imejikita katika ununuzi wa vifaa mbalimbali ikiwemo mabehewa, vichwa vya treni na mitambo ya matengenezo ya njia (on track machines) vitakavyotumika katika uendeshaji wa treni za SGR.

Manunuzi ya vifaa hivyo yamegawanyika katika makundi sita (6), kundi la kwanza linahusisha ununuzi wa vichwa vya treni vinavyotumia Dizeli, kundi la pili ni ununuzi wa vichwa vya treni vinavyotumia umeme (Electric Locomotive), kundi la tatu ni ununuzi wa treni za abiria zinazoenda kasi (EMU), kundi la nne ni ununuzi wa mabehewa ya abiria (passenger coaches), kundi la tano ni ununuzi wa mabehewa ya mizigo (Freight wagons) na kundi la sita ni ununuzi wa mitambo na mashine za matengenezo ya njia (on track machines).

Katika utekelezaji wa manunuzi ya vifaa mbalimbli vitakavotumika katika shughuli za uendeshaji wa SGR, hivi karibuni Juni 09, 2023. Shirika la Reli Tanzania lilipokea mabehewa sita (6) kati ya mabehewa thelathini (30) ya abiria yaliyofanyiwa ukarabati na maboresho na kampuni ya Lueckermier Transport and Logistics ya nchini Ujerumani na kurudi katika upya kwa zaidi ya asilimia 85.

Akinukuliwa wakati wa hafla ya mapokezi ya mabehewa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Bi. Amina Lumuli alisema

"Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Shirika la Reli Tanzania ilianza mchakato wa manunuzi ya vichwa viwili (2) vya treni na mabehewa thelathini (30) yaliyofanyiwa maboresho nchini Ujerumani ili kuweza kufanya majaribio ya miundombinu ya njia ya reli ya SGR na baadaye yatatumika kutoa huduma rasmi"

Mabehewa hayo sita (6) yenye ghorofa, manne (4) kati ni ya daraja la pili (2) yenye uwezo wa kubeba abiria 123 kila moja na mawili (2) ni daraja la tatu (3) yenye uwezo wa kubeba abiria 140 kila moja na yote yana uwezo wa kutembea mwendokasi wa kilomita 160 kwa saa. ndani ya mabehewa hayo kuna vifaa kama vile kiyoyozi (air condition), Runinga kwa ajili ya matangazo ya vituo mbalimbali vya treni inapopita na kamera za CCTV kwaajili ya usalama wa abiria na mazingira wakati wa safari.

Kuwasili kwa Mabehewa sita (6) ya ghorofa na pamoja na kuwasili kwa kichwa kimoja cha treni mwezi Julai mwaka huu inaashiria kuanza kwa shughuli za majaribio ya treni za SGR kipande cha kwanza Dar Es Salaam - Morogoro ifikapo mwezi Julai, 2023.

"Ukarabati wa vichwa viwili vya umeme yanaendelea kwenye karakana za Lueckemier Transport and Logistic GMBH Mukrani nchini Ujerumani, kichwa kimoja kipo katika hatua za mwisho za kufunga vifaa vya mawasiliano ya uendeshaji (On board Equipment - OBE) pamoja na kufunga vifaa vya umeme ambapo kazi hii inatarajiwa kukakimilika Juni, 2023, na tunatarajia kupokea kichwa kimoja na kingine kilichobaki kinategemewa kuwasili Novemba, 2023" alisema Kaimu Mkurugenzi Mkuu TRC Bi. Amina Lumuli.

Serikali kupitia TRC inaendelea kusimamia ununuzi wa mabehewa na vitendea kazi ili kuhakikisha vinafika kwa wakati kwa mujibu wa mikataba mbalimbali ya manunuzi'




BODI YA WAHARIRI
MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk, MHARIRI MSAIDIZI/MSANIFU | Sami Omary
HABARI | Hemed Mohamed, Mariam Kabange MAKALA | Aziza Charles, Amina Juma, Athumani Iddy
PICHA | Musa Kadiko, Hassan Mbonde, Augustino Bulegea